

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA YA  
ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

Anuani ya Simu: ELIMU DAR ES SALAAM.  
Simu: 2120402, 2120413,  
2120403/4/ 5/7/8/9  
Telex: 42741 Elimu Tz.  
Fax: 2113271 Elimu Tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. ED/OKE/NYE/VOL.1/14



S.L.P. 9121,  
DAR ES SALAAM.

Tarehe: 28/04/2011

Makatibu Tawala wa Mikoa  
Makatibu Tawala wa Wilaya  
Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Kanda  
Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Wilaya  
Maafisa Elimu wa Msingi/Sekondari wa Wilaya  
Wakuu wa Vyuo vya Ualimu  
Wakuu wa Shule za Sekondari  
Walimu Wakuu wa Shule za Awali/Msingi  
**TANZANIA BARA**

**MWONGOZO WA UVAAJI WA SARE ZA SHULE NA MWONEKANO NADHIFU WA  
WANAFUNZI/WANACHUO**


Kumejitokeza ukiukwaji wa sheria na kanuni za uendeshaji wa shule/vyuo hususan katika uvaaji wa sare za shule na usafi wa mwili. Baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakivaa sare zinazokiuka taratibu za shule, mfano, kuvaa nguo za kubana na fupi kwa wasichana na milegezo kwa wavulana. Aidha, baadhi ya wanafunzi wanafuga na kupaka rangi kucha, wanafuga ndevu, kuwa na nywele ndefu pamoja na mapambo mbalimbali.

Kutokana na kukithiri kwa hali hiyo katika baadhi ya shule, Wizara imelazimika kuwakumbusha walimu wakuu wa shule za msingi, wakuu wa shule za sekondari na vyuo vya Ualimu kuzingatia na kusimamia sheria na kanuni za uendeshaji wa shule/vyuo zilizopo ili kulinda maadili na nidhamu shuleni/vyuoni.

Kwa waraka huu, inaagizwa kuwa mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule ipasavyo, na awe nadhifu kwa kuwa na nywele fupi, kukata kucha, kutopaka rangi kucha, na kunyoa ndevu. Aidha, wasichana wawe na nywele fupi au kusuka nywele za mistari kwenda nyuma.

Mwongozo huu usomwe sambamba na mwongozo kuhusu uvaaji wa hijab na sala ya Ijumaa uliotolewa tarehe 18/08/1999.

**Mwongozo huu, unanza kutumika mara moja**

  
M. M. Wassena

**KAIMU KAMISHNA WA ELIMU**

**Nakala:**

1. Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI
2. Wakurugenzi wote, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi